**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**652** **ELIMU KWA MICHEZO**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka : 2011**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C** yenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vikokotozi **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (40 Alama)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Eleza maana ya usimamizi wa rasilimali katika michezo na umuhimu wake.
2. Taja michezo minne ya asili inayochezwa vijijini na eleza mchango wake katika malezi ya vijana.
3. Fafanua hatua nne muhimu za kufuata wakati wa kupiga penati katika mpira wa miguu.
4. Eleza sheria nne zinazotakiwa kuzingatiwa katika mchezo wa badminton.
5. Bainisha stadi nne za msingi katika mchezo wa mpira wa kikapu.
6. Eleza faida nne zinazopatikana kwa jamii kutokana na kuandaa mashindano ya michezo katika ngazi ya kijiji.
7. Changanua stadi nne zinazohitajika katika mchezo wa mpira wa mikono.
8. Eleza njia nne ambazo teknolojia ya mawasiliano imesaidia kukuza michezo ya kisasa.
9. Eleza mambo manne muhimu ya kuzingatia katika maandalizi ya mashindano ya shule.
10. Changanua njia nne zinazotumika na waamuzi katika mawasiliano ya michezo.

**SEHEMU B (30 Alama)**

Jibu maswali mawili katika sehemu hii

11. Eleza sababu tano zinazofanya michezo kuwa chombo cha mshikamano wa kitaifa.
12. Tathmini hatua tano zinazopaswa kufuatwa wakati wa kumpatia huduma ya kwanza mchezaji aliyepasuka mdomo.
13. Changanua mifumo mitatu ya kisasa ya mpira wa miguu na changamoto zake katika utekelezaji.

**SEHEMU C (30 Alama)**

Jibu maswali mawili katika sehemu hii

14. Eleza kanuni sita za usalama zinazopaswa kuzingatiwa katika michezo ya shule.
15. Jadili mchango wa utawala bora katika maendeleo ya michezo barani Afrika.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

16. Kwa mifano, eleza nafasi ya michezo ya asili katika kukuza tamaduni za taifa.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org